# Jarida la wiki
# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## Pongezi Mkurugenzi Jiji kwa kuchapa kazi - DC



"mimi nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze hadharani Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru. Mmepokea hapa taarifa, mmepokea changamoto lakini hazikusemwa vizuri huyu, mkurugenzi ameingia mfukoni kwake ametoa shilingi 12,000,000 kusaidia changamoto ya usafirishaji vifaa wakati ule wa mvua. Mafuru mimi nakupongeza sana. Sisi tunatamani Jiji la Dodoma liwe la mfano kwenye kutekeleza miradi, tunataka kuwa 'center of excellency' kwenye utekelezaji wa miradi"



*"Mimi na Watumishi wenzangu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma tupo tayari kuhesabiwa. Watanzania wenzangu msikose kuhesabiwa Tarehe 23 Agosti, 2022"*

## Hongera Rais Samia, barabara ya lami Nzuguni

## Asilimia 95 wanapata huduma ya maji Ntyuka







SIKU 7 ZA JIJI LA DODOMA

# Pongezi Mkurugenzi Jiji kwa kuchapa kazi - DC




**MHE. JABIR SHEKIMWERI**
**Mkuu wa Wilaya ya Dodoma**

Na. Dennis Gondwe, DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri amempongeza Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru kwa kutoa shilingi 12,000,000 kutatua changamoto ya usafirishaji wa vifaa wakati wa mvua kuvipeleka kwenye mradi wa ujenzi wa shule ya sekondari Hombolo Makulu.

Pongezi hizo alizitoa wakati akimkaribisha Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Dodoma kutembelea na kukagua shule hiyo.

Shekimweri alisema kuwa "na mimi nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze hadharani Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru. Mmepokea hapa taarifa, mmepokea changamoto lakini hazikusemwa vizuri huyu, mkurugenzi ameingia mfukoni kwake ametoa shilingi 12,000,000 kusaidia changamoto ya usafirishaji vifaa wakati ule wa mvua. Mafuru mimi nakupongeza sana. Sisi tunatamani Jiji la Dodoma liwe la mfano kwenye kutekeleza miradi, tunataka kuwa 'center of excellency' kwenye utekelezaji wa miradi alisema Shekimweri.

Mkuu huyo wa wilaya aliipongeza kamati ya ujenzi na walimu kwa kusimamia vizuri ujenzi wa shule hiyo. Alisema kuwa ushirikiano huo ndiyo umefanikisha kupiga hatua kubwa katika ujenzi huo.

Mradi huu utaajiri watu wengi. "Ajira ya mara moja inayoonekana ni ya walimu. Lakini tuna maabara, lazima tutaajiri wataalam wa maabara, tutakuwa na mafundi wateknolojia wa maabara. Lazima tuajiri mkutubi na wasaidizi, mpishi, boharia na mhasibu wa shule na ulinzi. Hivyo, ajira unaizungumzia katika mapana hayo. Kuna watakaoajiriwa ndani ya Hombolo Makulu na nje ya eneo hili" alisema Shekimweri.

Ujenzi wa shule ya sekondari katika kata ya hombolo makulu ulianza tarehe 25 Januari, 2022 kwa fedha kutoka mradi wa kuboresha elimu ya sekondari (SEQUIP) kwa gharama ya shilingi 600,000,000.



**JOSEPH MAFURU**
**Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma**

# Hongera Rais Samia, barabara ya lami Nzuguni

Na. Dennis Gondwe, DODOMA

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan amepongezwa kwa uongozi bora na kutoa fedha shilingi 6,109,748,702.50 za tozo ya Mafuta kujenga barabara ya Nzuguni - Mahomanyika kilometa 5.0 kwa kiwango cha lami.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Dkt. Damas Mkassa alipoongoza Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Dodoma kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Nzuguni Mahomanyika inayojengwa kwa kiwango cha lami.

Dkt. Mkassa alisema “nitangulize shukrani na pongezi kwa Rais, Samia Suluhu Hassan kwa uongozi bora na kazi nzuri. Fedha hizi nasikia zimetokana na tozo ya mafuta na kuna watu walikuwa wanapiga kelele juu ya tozo ila tunaona matokeo makubwa ya hizo tozo. Na siku zote mkuu wa nchi anapotoa maelekezo anakuwa ameona mbali. Tunaweza tusione matokeo mwanzo ila tunaweza kuona sasa hizi kilometa za barabara zinakwenda kujengwa hapa. Barabara hii ina umuhimu mkubwa sababu inatuunganisha na vitu vikubwa. Inatuunganisha na barabara kuu ya Dar es Salaam, inatuunganisha na Soko kuu la Job Ndugai, kutuo kikuu cha mabasi Dodoma hadi ‘ring road’ na hadi nyumba 350, ni muhimu sana kwa barabara hizi zinapokuwa katika jiji”.

Akiwasilisha taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Nzuguni Mahomanyika (kilometa 5.0) kwa kiwango cha lami, Mhandisi wa TARURA, Revocatus Nsubile alisema kuwa mradi huo upo chini ya Mkandarasi Nyanza Road Works co Ltd.

Alisema kuwa mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya shilingi 6,109,748,702.50. “Mkataba una miezi 12 na ulianza tarehe 5.4.2022 na unatarajiwa kukamilika tarehe 5.4.2023. Mradi una asilimia 28 zaidi ya asilimia 23 kiwango mradi uliotakiwa kuwa sasa. Hadi sasa hakuna mabadiliko ya gharama ya mradi na hatutarajii kuyapata” alisema Mhandisi Nsubile.

Akitoa ufafanuzi wa mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri alisema kuwa barabara hiyo ni ya kimkakati. “Mradi huu ulikuwa chini ya TARURA kwa ujenzi wa kilometa 1.55 lakini kwenye ziara ya Waziri wa Nchi- TAMISEMI, tuliweza kumpatia taarifa na nichukue nafasi hii kumpongeza Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde ambaye aliwasilisha ombi kwa serikali kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii kimkakati. Barabara hii inaunganisha mashamba ya mjini ‘urban farms’ ya Hombolo pamoja na Vikonje lakini inaunganisha makazi mapya yanayojengwa na TBA nyumba 350, lakini pia inatuunganisha na uwanja wa Ndege wa kimataifa wa Msalato ambao upo kwenye ujenzi. Babaraba hii inaunganisha na barabara ya Pete ya mzunguko, ni barabara inayotuunganisha na Soko Kuu la Job Ndugai, Kituo Kikuu cha Mabasi ya mikoani, lakini pia uwanja wa maonesho wa Nanenane lakini pia uwanja wa mpira utakaojengwa Nzuguni” alisema Shekimweri.

Mkuu wa wilaya aliitaja barabara hiyo kuwa ya kipekee. “Baada ya hoja hiyo, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo kwa TAMISEMI na waziri aliyatamka hapa kwamba tutaogezewe kilometa tano na hivyo, kujenga kwa kiwango cha lami nusu ya barabara hii kilometa 13. Ni matarajio yetu barabara hii ikikamilika kilometa 6.5 kwa bajeti inayokuja itaendelea kuwa kipaombele ili iweze kufikia matarajio ambayo kila mtu anayo” alisema Shekimweri.

Aidha, alimpongeza Diwani wa Kata ya Nzuguni kwa kazi nzuri na kutoa ushirikiano mkubwa kwenye kuwaelimisha wananchi kulinda mradi huo.

Jeremiah Chongo ambae ni mkazi wa Mahomanyika alisema kuwa barabara hicho itachangia kukuza uchumi wa maeneo mbalimbali ya jiji hilo. Alisema kuwa ujenzi wa barabara kama ulivyo ujenzi wa miundombinu mingine ni kichocheo cha maendeleo ya maeneo mbalimbali kwa sababu inafungua fursa za kibiashara.



**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN**
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



**DKT. DAMAS MKASSA**
**Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi CCM Mkoa wa Dodoma**

# Jiji lajenga vituo vya afya vi3

## *kwa mapato ya ndani*



**MRADI WA KITUO CHA AFYA NKUHUNGU**

Na. Dennis Gondwe, DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imepongezwa kwa ujenzi wa vituo vitatu vya afya kutoka mapato ya ndani kwa lengo la kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, Dkt. Damas Mkassa alipoongoza Kamati ya Siasa Mkoa wa Dodoma kutembelea na kukagua ujenzi wa kituo cha Afya Nkuhungu kilichopo jijini hapa.

Dkt. Mkassa alisema "niipongeze Halmashauri ya Jiji la Dodoma ikijumuisha wewe mwenyewe msimamizi mkuu wa wilaya, Mkurugenzi wa Jiji, Mganga Mkuu kwa kazi mliyonayo katika ujenzi wa vikuo vitatu vya afya kutoka mapato ya ndani. Si jambo la mchezo kwamba halmashauri imeweza kubeba ujenzi wa vituo vitatu vya afya kwa wakati mmoja, hatua hii ni nzuri. Sidhani kama nina maneno mengi ya kusema bali kuhimiza ile kasi iliyoanza isife. Nkuhungu hatuna zahanati wala kituo cha afya".

Mwenyekiti huyo alishauri kuwa mfumo wa malipo utakapofunguliwa kipaombele kiwe ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto. "Nkuhungu na Chang'ombe tunachuana kwenye 'reproduction'. Ni watu wenye shughuli nyingi, tupo 'busy' sana lakini hiyo ni kazi yetu sisi wazazi, uchungu wa mwana aujuae mzazi" alisema Dkt. Mkassa.

Akiwasilisha taarifa ya ujenzi wa Kituo cha Afya Nkuhungu, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dkt. Andrew Method alisema kuwa ujenzi ulianza kwa fedha za mapato ya ndani. Alisema kuwa serikali ilielekeza jiji kujenga vituo vya afya vitatu kwa mapato ya ndani. "Kituo kingine ni Kizota pamoja na Zuzu. Mradi ulianza kutekelezwa tarehe 17/3/2022. Jiji lilileta shilingi 207,900,000 kwa ajili ya ujenzi wa majengo haya na awamu hii tunajenga jengo la Wagonjwa wa Nje na Maabara. Awamu ya pili tutajenga jengo la upasuaji, jengo la kina Mama na Kichomea taka pamoja na njia za kuunganisha majengo haya" alisema Dkt. Method.

Alisema kuwa mradi huo ni muhimu kwa sababu utahudumia wananchi 38,000 kutokana na eneo hilo halikuwa na huduma za afya pamoja na kuwa na watu wengi. "Katika kituo hiki tutaweka mifumo ya kisasa ya kuhudumia wagonjwa. Tumeshaanza kuisimika, itakapokamilika wagonjwa wataanza kuonwa kwenye mifumo ya kieletroniki badala ya 'paper work' tulizozizoea" alisema Mganga Mkuu.



# **Tupande** miti ya matunda kuboresha lishe



Na. Dennis Gondwe, DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri ameshauri miti ya matunda kupandwa katika shule ya sekondari Hombolo Makulu inayojengwa ili kuitikia agenda ya lishe wilayani humo.

Shekimweri alishauri hilo wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma iliyofanya ziara ya kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa shule ya sekondari Hombolo Makulu.

Shekimweri alisema kuwa eneo la shule hiyo lipandwe miti ya matunda ili kuchochea masuala ya Lishe bora. "Tunataka watoto wakitoka nje wakutane na maua wajifunze kupenda bustani na wajifunze kupenda kupanda miti. Na eneo hili itapandwa miti mchanganyiko hasa ya matunda. Miti hiyo ni kujibu agenda ya lishe wilayani Dodoma. Miti ya matunda, miti ya vivuli na huko kwenye vivuli tuweke na vimeza vya kusomea. Watoto wakipigwa na mitihani wapate hewa safi ya 'oxygen' na maarifa ndiyo yataweza kuingia vizuri" alisema Shekimweri.

Alisema kuwa shule nzuri ya aina ile yenye majengo mengi yaliyopangiliwa vizuri haitoshelezi kama haitakuwa na mandhari nzuri. "Tumeshaanza kupanda miti hapa na tutaendelea kuipanda. Baada ya kufanya usafi na leveling hapa, mimi nikuhakikishie hapa tutaweka bustani nzuri" alisema Shekimweri.

Nae mzazi Agatha Kihori alisema kuwa wananchi wengi hawana uelewa wa masuala ya lishe jambo linaloendea kudumaza hali ya lishe katika kata yao.



# Hospitali ya Wilaya kujengwa Dodoma




JABIR SHEKIMWERI
Mkuu wa Wilaya ya Dodoma

Na. Dennis Gondwe, DODOMA

WILAYA ya Dodoma imemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia fedha shilingi 500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya ili kusogeza huduma bora za afya karibu na wananchi.

Pongezi hizo zilitolewa na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma ilipotembelea na kukagua ujenzi wa Kituo cha Afya Chang'ombe.


Shekimweri alisema "hapa Dodoma hatuna hospitali ya wilaya, nichukue nafasi hii kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha shilingi 500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya wilaya pale Nala. Hatujaanza ujenzi sababu tumeomba idhini ya kujenga hospitali ya ghorofa. Nimshukuru Mganga Mkuu wa Jiji, Dkt. Andrew Method pamoja na wenzake hasa katika mazingira haya ambayo hatuna hospitali ya wilaya, Kituo cha Afya Makole kinafanya kazi kubwa kutusaidia kwa matibabu ya wagonjwa wa ndani".

Mkuu huyo wa wilaya alisema kuwa wameshapokea watumishi wa Afya 18. "Namshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia watumishi wapya. Katika kituo hiki wameshapangwa watumishi 12, kwa hiyo, Mheshimiwa Diwani lile ombi lako kituo cha Afya kinakamilika hakina watumishi Rais Samia keshalijibu. Naomba mupokee vizuri kama ulivyo mkarimu na wenzako muwapokee na kukaa nao kwa wema" alisema Shekimweri.

Akiwasilisha maelezo ya mradi huo, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dkt Andrew Method alisema kuwa mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili. "Awamu ya kwanza tulipokea shilingi 250,000,000 zilizojenga jengo la wagonjwa wa nje, maabara na kichomea taka. Kazi imekamilika kwa 99%. Awamu ya pili tumepokea shilingi 250,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la kina mama, jengo la upasuaji na jengo la kufulia. Ujenzi umeanza, tupo katika hatua ya msingi" alisema Dkt. Method.

Alisema kuwa ujenzi huo ukikamilika utahuduma wananchi karibu 30,000 waliokuwa wakizifuata huduma za afya Kituo cha Afya Makole. Alisema kuwa kituo cha Afya Makole kimekuwa na msongamano mkubwa wa wananchi wanaoenda kupata huduma hapo. "Tunatarajia kuanza kutoa huduma mwishoni mwa mwezi huu tarehe 29 baada ya kukamilisha uwekaji wa vifaa tiba na samani katika kituo hiko" alisema Dkt. Method.

Ujenzi wa Kituo cha Afya Chang'ombe ulianza tarehe 24 Desemba, 2021 kwa fedha za tozo kutoka serikali kuu.




# SIKU 7
## ZA JIJI LA DODOMA

JARIDA HILI LINATOLEWA NA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

S.L.P 1249 DODOMA, TANZANIA
Baruapepe: cd@dodomacc.go.tz
Tovuti: www.dodomacc.go.tz